



Jimbo la Vermont Idara ya Usalama wa Umma

Mpango wa Ufikiaji wa Huduma za Lugha

Kichwa cha Waraka: Mpango wa Ufikiaji wa Huduma za Lugha wa DPS

Tarehe ya Masahihisho: 15/12/2021

Nambari ya Masahihisho: 2

Waandishi: Dorf, Lee; Kessler, Barbara; Fox, Mourning; Nasreddin-Longo, Etan, White, Wilda; Morrison, Jennifer

Aina ya Waraka: Mpango

Hali ya Waraka: Mwisho

Imeidhinishwa na: Michael Schirling, Kamishna

Iliidhinishwa mnamo: 05/01/2022

Sahihi: _____

A handwritten signature in black ink, appearing to be "Michael Schirling", written over a horizontal line.

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

Jedwali la Yaliyomo

REKODI YA MASAAHIHISHO YA MPANGO	4
VITENGO NA AKRONIMI ZA IDARA	5
I. FAFANUZI	5
II. UTANGULIZI	6
III. MADHUMUNI NA UPEO	7
IV. USULI	7
V. UCHANGANUZI WA MAMBO MANNE	8
VI. MAWASILIANO KATI YA WATU WA DPS NA LEP	8
VII. AINA ZA USAIDIZI WA LEP ZILIZOPO	10
A. HUDUMA ZA TAFSIRI NA UKALIMANI	10
B. HUDUMA ZA UKALIMANI	12
C. LUGHA YA ISHARA	13
D. SEHEMU ZA KUJIBU USALAMA WA UMMA WA VERMONT (VERMONT PUBLIC SAFETY ANSWERING POINTS, PSAPS)	13
E. GOOGLE NA HUDUMA NYINGINE ZA TAFSIRI ZA KIOTOMATIKA	14
F. WAAJIRIWA WA LUGHA MBILI	14
VIII. KUTAMBUA MAHITAJI YA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA	14
IX. MAWASILIANO YA LUGHA RAHISI	14
X. MBINU MBADALA ZA MAWASILIANO	14
XI. UFAAFU WA MILA NA ISIMU	15
XII. MAFUNZO YA WAFANYAKAZI	15
XIII. MAJUKUMU YA WAFANYAKAZI	15
XIV. UHIFADHI WA REKODI	16
XV. KUFUATILIA NA TATHMINI	16
XVI. TAFSIRI YA NYARAKA MUHIMU	16
XVII. UTAYARI WAKATI WA DHARURA	16
XVIII. UHAMASISHAJI NA UFAHAMU WA UMMA KUHUSU HUDUMA ZA UFIKIAJI WA LUGHA	17
XIX. UTARATIBU WA MAONI NA MALALAMISHI YA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA	17
XX. MRATIBU WA TITLE VI	18
KIAMBATISHO A: SERA YA HUDUMA ZA UKALIMANI YA VSP-DIR-425	21
KIAMBATISHO B: FOMU YA MALALAMISHI YA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA	23
KIAMBATISHO C: FOMU YA IDARA YA UFUATILIAJI WA USAIDIZI WA LUGHA YA USALAMA WA UMMA	25

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

KIAMBATISHO D: FOMU YA OMBI LA MKALIMANI YA AALVI 27

KIAMBATISHO E: VITUO VYA UMMA VYA DPS 28

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

REKODI YA MASAHISHO YA MPANGO

Tarehe ya Masahisho	Muhtasari wa Mabadiliko	Kurasa Zilizoathiriwa	Ilikamilishwa na
15/11/2021	Mpango wa kwanza	Zote	Lee Dorf
30/12/2021	Uhariri	Zote	Wilda White na Jen Morrison

VITENGO NA AKRONIMI ZA IDARA

Akronimi	Idara
DFS	Kitengo cha Usalama wa Moto cha Vermont
DPS	Idara ya Usalama wa Umma
DPS-CO	Idara ya Usalama wa Umma – Ofisi ya Kamishna
F&A	Kitengo cha Fedha na Utawala
RTS	Huduma za Teknolojia za Redio ya Vermont
VCIC	Kituo cha Habari za Uhalifu cha Vermont
VEM	Udhibiti wa Hali ya Dharura wa Vermont
VFL	Maabara ya Uchunguzi ya Vermont
VSP	Polisi ya Jimbo la Vermont

I. FAFANUZI

Mbinu mbadala za mawasiliano inamaanisha mbinu za kuwasilisha ujumbe unaojaliza au kubadilisha mbinu za kawaida za mawasiliano ya mdomo na ya maandishi. Madhumuni ya mbinu hizi ni kuwafikia vyema wale walio na kasoro za lugha ya mdomo, lugha ya maandishi au ulemavu mbalimbali. Mifano ya mbinu mbadala za mawasiliano ni pamoja na vielezo vya michoro, video, rekodi za sauti na lugha ya ishara. Mbinu mbadala ya mawasiliano inayofaa itategemea na mahitaji ya hadhira.

Utamaduni inamaanisha tabia, imani, maadili, mitazamo, maana na ishara za kundi la watu. Utamaduni unaweza kujumuisha mambo mbalimbali ikiwemo umri, asili ya taifa, kiwango cha elimu, hali ya ajira, aina ya familia, aina ya kaya, jinsi, kizazi, eneo la kijiografia, hali ya uhamiaji, mapato, lugha, kiwango cha kujua kusoma na kuandika, tajriba ya jeshi, hali ya uzazi, uwezo wa kimwili, uwezo wa utambuzi, imani za kisiasa, mbari, kabila, dini na mvuto wa jinsia.

Inayofaa kimila na kiisimu inamaanisha huduma ambazo zinaheshimu na kukubali tamaduni, imani na maadili ya mtu.

Mpango ya DPS inamaanisha hali ya kawaida ya kuwaweka wafanyakazi kwenye idara nzima na ni pamoja na shughuli zote na sehemu za kazi za Idara ya Usalama wa Umma. Kwa Mpango huu na kulingana na sera ya idara ya VI/LEP, wakuu wa idara na kitengo wanawajibikia kuamua jinsi watakavyotekeleza Mpango huu. Hii inapaswa kujumuisha utekelezaji kwenye ngazi zote za kitengo ambapo huduma zinazowafaidi watu kwa LEP zinatolewa.

Kwa mfano, viongozi wa kitengo wanaweza kuchagua kuratibu utekelezaji wa Mpango huu kwenye ngazi za kitengo, ofisi, mpango au sehemu.

JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA

Wajiriwa wa lugha mbili inamaanisha wajiriwa wanaohudumu katika cheo cha lugha mbili kilichoteuliwa walio na wajibu wa kutafsiri nyaraka au kutoa huduma za ukalimani kwa lugha iliyobainishwa katika maelezo ya cheo chao.

Mawasiliano ya kufaa inamaanisha mawasiliano yanayotosha kumpa mtu wa LEP kiwango sawa cha ufikiaji wa huduma ambazo watu ambao si wa LEP wanapata.

Usaidizi wa Kifedha Kupitia Serikali Kuu unajumuisha, lakini si tu, ruzuku na mikopo ya fedha za serikali kuu; ruzuku au michango ya mali ya serikali kuu; mafunzo; maelezo ya mhudumu wa serikali kuu; au makubaliano, mpango wowote au kandarasi nyingine ambayo ina kama moja ya madhumuni yake kuwa utoaji wa usaidizi.

Ukalimani unamaanisha mawasiliano ya papo hapo kwa njia ya mdomo (au alama) ya maana kutoka lugha moja (lugha chanzo) hadi nyingine (lugha lengwa). Ujumbe unawasilishwa kwa njia ya mdomo. Huduma za ukalimani zinazotokea kwa njia ya simu zinaitwa huduma za ukalimani za mawasiliano ya simuni.

Ufasaha Mdogo wa Kiingereza (LEP) inamaanisha watu wasiozungumza Kiingereza kama lugha yao ya msingi, huzungumza Kiingereza chini ya “vizuri sana,” na/au walio na uwezo kidogo wa kusoma, kuzungumza, kuandika au kuelewa Kiingereza.

Ufikiaji muhimu inamaanisha usaidizi wa lugha unaosababisha mawasiliano sahihi, ya wakati na yanayofaa bila gharama kwa mtu aliye na LEP. Kwa watu wa LEP, ufikiaji muhimu unamaanisha ufikiaji ambao haujawekewa vikwazo zaidi, haujacheleweshwa, wala duni ukilinganishwa na mipango au shughuli zinazopewa watu walio na ufasaha wa Kiingereza.

Umma inamaanisha mtu yeyote wa umma bila kujali eneo la kijiografia ndani ya Vermont au hali ya uraia. Umma unajumuisha watu wote wa Marekani bila kujali uraia wala eneo la kijiografia.

Tafsiri inamaanisha ubadilishaji wa mawasiliano ya maandishi kutoka lugha moja (lugha chanzo) hadi lugha nyingine (lugha lengwa) kwa njia ya maandishi. Tafsiri sahihi ni ile inayowasilisha maana iliyokusudiwa na muhimu ya matini asili.

Nyaraka muhimu ni karatasi au maudhui ya maandishi ya elektroniki yaliyo na maelezo ambayo ni muhimu kwa ajili ya kufikia mpango au maelezo au yanahitajika kisheria kusambazwa hadharani na DPS. Hizi zinaweza kuwa nyaraka, fomu, matangazo na nyenzo nyingine. Iwe waraka (au maelezo ambayo unaomba) ni "muhimu" au si muhimu inategemea umuhimu wa mpango, maelezo, mkutano, au huduma husika na madhara kwa watu walio na LEP ikiwa maelezo yanayosemwa hayajatolewa kwa usahihi au kwa wakati.

II. UTANGULIZI

Jimbo la Vermont Department of Public Safety (DPS) linaahidi kutoa ufikiaji kwa wakati, wa ubora wa juu na muhimu kwa mipango ya DPS na huduma kwa watu walio na ufasaha kidogo wa Kiingereza (LEP) Mpango huu wa Ufikiaji wa Huduma za Lugha (Plan) unakusudiwa kukuza mawasiliano yanayofaa kati ya DPS na watu walio na LEP.

Mpango huu uliundwa kwa kutumia [Idara ya Tathmini ya Ufikiaji wa Huduma za Lugha ya Haki na Chombo cha Kupanga kwa ajili ya Mipango Inayoendeshwa na Kusaidiwa na Serikali Kuu](#), na unaelezea mikakati ya DPS ya kuhakikisha ufikiaji wa huduma za lugha inavyohitajika na

JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA

Title VI ya Sheria ya Haki za Raia ya 1964, Amri ya Rais 13166, Sehemu ya 1557 ya Sheria ya Utunzaji wa Gharama Nafuu na kanuni zake za utekelezaji (42 C.F.R. §92).

Vilevile, DPS imeahidi kutoa mawasiliano yanayofaa kwa watu walio na ulemavu. Miongozo na rasilimali nyingi zilizojumuishwa katika Mpango huu zinaweza kutumika kuhakikisha mawasiliano yanayofaa na watu walio na ulemavu.

DPS itapitia Mpango huu kila mwaka na itasasisha mikakati ili kuendeleza ahadi ya idara ya kutoa huduma na maelezo yanayoweza kufikiwa na yanayofaa kimila na kiisimu.

III. MADHUMUNI NA UPEO

Mpango wa ufikiaji wa huduma za lugha ni waraka unaobainisha jinsi ya kutoa huduma kwa watu ambao hawazungumzi Kiingereza au wana ufasaha kidogo wa Kiingereza. Mawasiliano yanayofaa ni muhimu kwa utoaji wa huduma za ubora wa juu na za usawa. Utegemeaji wa watu wasiohitimu kukalimani maelezo unaweza kusababisha kuelewa visivyo au matokeo ya kusikitisha. Mpango wa ufikiaji wa huduma za lugha unaweza kusaidia kuhakikisha kuwa shirika linatoa huduma za lugha zinazofaa. Mpango wa ufikiaji wa huduma za lugha pia unaweza kusaidia kuhakikisha kuwa wafanyakazi wa shirika wanafahamu cha kufanya wakati mtu aliye na ufasaha kidogo wa Kiingereza anahitaji usaidizi.

Mpango huu unatumika kwenye vitengo na sehemu zote za Idara ya Usalama wa Umma. Kufuata miongozo hii ni muhimu kwa mafanikio ya dhamira yetu ya kukuza ugunduzi na uzuiaji wa uhalifu, kushiriki katika utafutaji wa watu waliopotea na kutoweka na kusaidia katika kesi za jimbo zima au majanga au dharura za ndani.

IV. USULI

Tangu mwisho wa karne ya 20, Vermont imeshuhudia ongezeko bayana la idadi ya watu wanaozungumza lugha ambayo si Kiingereza. Takwimu za taifa zinabainisha kwamba miongoni wa Wamarekani walio na miaka mitano au zaidi, asilimia 8.4 wanazungumza Kiingereza chini ya “vizuri sana”, ambao ni msamiati na kipimo kinachotumika kuelezea wale walio na Ufasaha Kidogo wa Kiingereza (LEP).¹ Katika jimbo la Vermont, wakazi na wageni wa LEP wanaishi na kutembea jimbo zima, huku idadi kubwa ikiwa katika maeneo yaliyo na idadi kubwa.

Kihistoria, nyaraka rasmi zingehitajika tu kutafsiriwa kwa Kifaransa na Kihispania, lakini wakazi wa Vermont sasa wanahitaji ufikiaji wa maudhui na huduma katika zaidi ya lugha 13. Mbali na Kiingereza, Kifaransa na Kihispania, idadi kubwa ya wakazi wa Vermont na wageni ambao huenda wakahitaji huduma za DPS sasa pia wanazunguma Kiarabu, Kibama, Kichina, Kirundi, Kilingala, Kinepali, Kisomali, Kiswahili na Kivietnamu.

Kiingereza cha kuzungumzwa huenda pia yasiwe mawasiliano yanayofaa kwa wale ambao hawana uwezo wa kusikia au walio na matatizo ya kusikia, wengi wao hutumia Lugha ya Ishara ya Marekani (ASL) kama lugha yao ya msingi.

Kaunti tano za Vermont zilizo na watu wengi wa LEP ni Chittenden, Franklin, Rutland, Washington na Windsor. Kulingana na makadirio ya 2015, lugha zilizoenea sana Vermont

¹ [Utafiti wa Jamii ya Marekani, Makadirio ya Miaka 5, 2015-2019](#)

JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA

miongoni mwa watu wa LEP ni Kifaransa, Kihispania, lugha Nyingine za Kihindi¹, Kichina na Kivietnamu. Asilimia arubaini ya wakazi wa Vermont walio na ufasaha wa Kiingereza wanazungumza lugha mbali na lugha zilizotajwa ambazo zimeorodheshwa.²

V. UCHANGANUZI WA MAMBO MANNE

Kwa sababu kuna lugha nyingi za msingi zinazozungumzwa Vermont, DPS itatumia uchanganuzi wa mambo manne uliobainishwa katika Mwongozo wa Idara ya Haki ya Marekani (DOJ) kwa Wapokeaji Usaidizi wa Fedha za Serikali Kuu, unaopatikana kwenye tovuti ya DOJ, ili kuamua mikakati ambayo itatoa ufikiaji muhimu wa huduma na mipango yake.

DPS inatambua kwamba mawasiliano na DPS na vitengo vyake yatatofautiana sana. Kwa hivyo, lazima uchanganuzi wa mambo manne uendelee kubadilika na utahitaji usawazishaji ulipo wa mambo manne ambayo ni:

- Idadi au uwiano wa watu wa LEP wanaostahiki kuhudumiwa au wanaoweza kukumbana na wafanyakazi wa DPS au wanaoweza kunufaika kutokana na mipango au huduma ndani ya mamlaka ya DPS au sehemu fulani ya kijiografia.
- Mara ambazo watu wa LEP wanaweza kukutana na wafanyakazi, mipango au huduma za DPS.
- Hali na umuhimu wa mawasiliano, mpango, maelezo au huduma inayotolewa.
- Gharama ya kutoa usaidizi wa LEP na rasilimali zilizopo.

VI. MAWASILIANO KATI YA WATU WA DPS NA LEP

Jedwali lifuatalo linatambua kulingana na kitengo, miingiliano inayowezekana zaidi kati ya watu wa LEP na wafanyakazi, mipango au huduma za DPS.

	DPS	VSP	VEM	DFS	VFL	VCIC	RTS
TOVUTI NA MITANDAO YA JAMII	Tovuti	Tovuti	Tovuti	Tovuti	Tovuti	Tovuti Tovuti ya Sajili ya Wahalifu wa Ngoni	Tovuti
	Mitandao ya Jamii	Mitandao ya Jamii	Mitandao ya Jamii	Mitandao ya Jamii			
VITUO VYA UMMA	Simu ya Umma	Simu ya Umma	Simu ya Umma	Simu ya Umma		Simu ya Umma	
	Afisi	Afisi za Uwanjani		Afisi za Kieneo		Afisi Isiyo na Kambarau	

¹ Pia zinaitwa lugha za Indo-Aryan, <https://www.britannica.com/topic/Indo-Aryan-languages>

² [Idadi ya Watu wa LEP katika Ramani za Vermont 2015 katika Jamii Yako – Idadi kulingana na Kaunti](#)

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

	DPS	VSP	VEM	DFS	VFL	VCIC	RTS
DHARURA		9-1-1	Arifa ya VT				
UTEKELEZAJI		Utekelezaji wa Uwanjani		Utekelezaji wa Msimbo wa Jengo na Huduma za Usalama			
		Mahojiano ya Uchunguzi Uwanjani					
		Kumhoji Mshukiwa					
		Miadi					
UHAMASISHAJI, MAELEZO, ELIMU		Malalamishi					
		Uhamasishaji wa Jamii	Rasilimali na Machapisho	Mafunzo na Mazoezi	Elimu ya Umma na Maelezo ya Uhamasishaji	Maelezo ya Historia ya Mhalifu – Uchunguzi wa Rekodi	
VIBALI, LESENI		Vibali		Vibali, Leseni za Biashara, Vyeti na Ubadilishaji			
SAJILI						Sajili ya Mhalifu wa Ngono	

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

	DPS	VSP	VEM	DFS	VFL	VCIC	RTS
KAMATI NA BODI	<ul style="list-style-type: none"> ▪ Bodi ya Ushauri wa Utekelezaji wa Sheria ▪ Tume ya Ushauri wa Polisi ya Jimbo ▪ Baraza la Ushauri wa Mawasiliano ya Dharura ▪ Bodi ya Ushauri wa VIBRS ▪ Baraza la Ushauri wa Utayari wa Dharura wa Gavana ▪ Bodi ya Uongozi wa VALCOUR 						

Ingawa mawasiliano, huduma na haki zote za watu ni muhimu, DPS itatumia uchanganyuzi wa mambo manne kuipa kipaumbele huduma kwa watu wa LEP ili huduma kama hizo zilengwe pale zinapohitajika zaidi, kulingana na hali na umuhimu wa shughuli ya DPS husika.

VII. AINA ZA USAIDIZI WA LEP ZILIZOPO

A. HUDUMA ZA TAFSIRI NA UKALIMANI

Jimbo la Vermont lina kandarasi za jimbo zima za huduma za tafsiri na ukalimani na (1) Corporate Translation Services Inc. (dba [Language Link](#)); (2) [Telelanguage Inc.](#); na (3) [Worldwide Interpreters Inc.](#) Kandarasi zinaweza kupatikana kwenye ukurasa wa Buildings and General Services (BGS) Current Statewide Contracts, chini ya "[Translation & Interpretation Services.](#)"

Baada ya ombi, lugha zifuatazo zinaweza **kutafsiriwa**:

Kihispania	Kiitaliano	Kifaransa	Kijerumani	Kireno
Kialbania	Kibulgaria	Kiserbia-Kikroeshia (Kibosnia, Kiserbia na Kikroshia)	Kicheki	Kidachi
Kifini	Kigiriki	Kiebrania	Kihungaria	Kipolandi
Kirusi	Kiarabu	Kibama	Kifarsi	Kijapani
Kinepali	Kichina (Kimandarini na Kikantoni)	Kikorea	Kivietnamu	Kituruki

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

Kiakani	Kiamhariki	Kimei	Kitigrinya	Kiswahili
Kisomali	Kitwi	Kiafmaksaa	Kirundi	Kihmongi
Kitagalogi				

Lugha ambazo hazijaorodheshwa zinaweza kuombwa na wakandarasi wanatarajiwa kutoa watafsiri waliohitimu.

Tafsiri zitatolewa kwa nyakati zifuatazo: hadi maneno 2,000 (siku mbili); maneno 2,000 – 2,000 (siku nne), zaidi ya maneno 4,000 (hadi siku tano).

Kwa matukio kama vile majanga ya asili au dharura za afya, wakandarasi wanaweza kutoa huduma za haraka ndani ya saa 24.

Baada ya kuomba, lugha zifuatazo zinaweza **kukalimaniwa**:

Kiarabu	Kibosnia	Kibama	Kichina (Kimandarini, Kikantoni)	Kifaransa
Kirundi	Kikareni	Kimei	Kinepali	Kirusi
Kisomali	Kiafmaksaa	Kihispania	Kiswahili	Kivietnamu

Lugha ambazo hazijaorodheshwa zinaweza kuombwa na wakandarasi wanatarajiwa kutoa wakalimani waliohitimu.

Mashirika haya pia yanaweza kutoa huduma za ukalimani wa simu na video. Orodha ya lugha inaegemea sana ukalimani, ingawa lugha ambazo hazijaorodheshwa zinaweza kutolewa ikiwa zipo zinapohitajika.

Huduma za mkalimani kupitia kampuni hizi zinaweza kutolewa kupitia nambari ya dharura isiyo ya malipo saa ishirini na nne kila siku ya mwaka.

Mtoa Huduma	Nambari ya Mawasiliano
Language Link	855-295-9177
Telelanguage	888-983-5352
Worldwide Interpreters	866-967-5313

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

B. HUDUMA ZA UKALIMANI

Kandarasi za Jimbo la Vermont na kampuni mbili za ziada ili kutoa huduma za mkalimani wa ana kwa ana.

Mtoa Huduma	Nambari ya Mawasiliano
Association of Africans Living in Vermont	802-985-3106
US Committee for Refugees & Immigrants	802-654-1700

Association of Africans Living in Vermont Inc. (AALV) na US Committee for Refugees & Immigrants itatoa huduma za ukalimani wa ana kwa ana zinapohitajika kwa lugha zifuatazo:

Kiarmenia	Kiamhariki	Kiarabu	Kibosnia	Kibhutani
Kibama	Kichina (Kikantoni)	Kichina (Kimandarini)	Kikrioli cha Haiti	Kidinka
Kifaransa	Kihindi	Kikareni (S’gaw)	Kibembe	Kikongo
Kirundi	Kinyarwanda	Kiswahili	Kilingala	Kimaimai
Kinepali	Kireno	Kiromania	Kirusi,	Kiserbia- Kikroeshia
Kisomali	Kihispania	Kitibeta	Kituruki	Kivietnamu

Kila kampuni inahitaji muda wa siku tano za kazi, ili kutoa huduma na kila mkalimani anaweza kutumiwa hadi saa tatu mfululizo. Baada ya saa tatu mfululizo, mkalimani tofauti lazima atumiwe. Huduma zinaweza kutolewa wakati wa saa za kufanya kazi za kawaida na zisizo za kawaida.

Kampuni pia zina kandarasi ya kutoa huduma za ukalimani wa ana kwa ana katika hali za dharura ikiwa wakalimani waliohitimu wapo.

Maombi ya huduma za ukalimani kwa Kamati ya Wakimbizi na Wahamiaji ya Marekani yanaweza kutumwa kwa RequestInterpreterVT@uscmail.org.

Maombi ya huduma za ukalimani kwa AALVI yanafanywa kwa kukamilisha fomu ya Ombi la Mkalimani ([Kiambatisho D](#)).

Kandarasi kwa AALV na Kamati ya Wakimbizi na Wahamiaji ya Marekani zinaweza kupatikana kwenye Tovuti ya [Tovuti ya Kandarasi ya BGS](#).

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFUKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

C. LUGHA YA ISHARA

Jimbo la Vermont pia linashirikiana na Vancro Integrated Interpreting Services (VIIS), huduma ya rufaa ya ukalimani wa lugha ya ishara ya Marekani, kufanya mikutano, miadi, shughuli, n.k., kufikiwa na watu ambao wana ulemavu wa kusikia au matatizo ya kusikia na wanaotumia lugha ya ishara ya Marekani kuwa njia yao ya msingi ya mawasiliano.

VIIS pia inaweza kutoa huduma za Lugha ya Ishara ya Kinepali.

Huduma zinaweza kuombwa ifuatavyo:

Barua pepe	interpretingservices@vancro.com
Fomu ya ombi mtandaoni (inahitaji jina la mtumiaji na nenosiri)	https://vancrois.com/request-interpreter.html

D. SEHEMU ZA KUJIBU USALAMA WA UMMA WA VERMONT (VERMONT PUBLIC SAFETY ANSWERING POINTS, PSAPS)

Sehemu ya kujibu usalama wa umma (PSAP) ni kituo kilicho na uwezo wa kupokea simu za dharura, zinazofanya kazi saa ishirini 24, zilizopewa jukumu la kupokea simu za 9-1-1 na kupeleka, kuhamisha, au kuwasilisha simu za dharura za 9-1-1 kwenye shirika jingine la usalama wa umma au mashirika ya usalama ya binafsi.

Vermont Public Service Answering Points (PSAPs) inaweza kuunganisha haraka huduma kupitia Telelanguage, Inc.

Kila PSAP na pia University of Vermont Dispatch, ina nambari yake maalum ya simu ya kutumia kwa madhumuni ya ufuatiliaji wa data.

Huduma za ukalimani zinazopatikana kupitia PSAP zinatumiwa si tu na VSP, bali pia mashirika mengine ya utekelezaji sheria ya Vermont. VSP hushughulikia gharama zote zinazohusiana na simu hizo.

Zifuatazo ni nambari maalum za simu za PSAP:

**Sehemu za Kujibu Usalama wa Umma
wa Vermont**

Hartford
Lamoille County
Saint Albans
Shelburne
University of Vermont Dispatch
Westminster
Williston

Nambari Maalum ya Simu

844-459-7503
844-463-9166
844-567-7289
844-670-9883
844-612-7353
844-627-9693
844-464-1151

E. GOOGLE NA HUDUMA NYINGINE ZA TAFSIRI ZA KIOTOMATIKI

Kwa sasa, tovuti za DPS, VEM, na VSP zinatumia kipengele cha Google Translate, kinachotoa tafsiri ya kiotomatiki ya maudhui ya tovuti hadi katika lugha zaidi ya 100. Google Translate haina mtiririko; kwa lugha ambazo si maarufu sana, tafsiri zinaonekana kuwa sisisi na maana nyingine zinaweza “kupotea katika tafsiri.” Hata hivyo, wakati mwingine, manufaa ya Google Translate yanazidi hatari za tafsiri zenye makosa.

DPS inaweza kutumia huduma za tafsiri za kiotomatiki kupitia huduma nyingine za tafsiri za ndani ya programu, kama vile zile zilizopachikwa katika mifumo ya mitandao ya jamii.

F. WAAJIRIWA WA LUGHA MBILI

Wajiriwa wa lugha mbili wanaweza kutoa huduma za usaidizi wa lugha wakati wa hali za dharura au muhimu inavyohitajika. Wajiriwa wa lugha mbili si wakalimani walioidhinishwa.

VIII. KUTAMBUA MAHITAJI YA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA

DPS itakuwa na kadi za “I Speak” katika angalau lugha za Makundi yote ya Lugha ya LEP yaliyopo ili kusaidia watu wa LEP kutambua mahitaji yao ya ufikiaji wa huduma za lugha kwenye maeneo yote ambapo watu wa LEP wanatarajiwa kutangamana na DPS mara kwa mara. DPS pia itakuwa na taarifa zilizochapishwa mapema katika lugha zote za Makundi ya Lugha ya LEP ambazo mwajiriwa wa DPS anapanga ufikiaji wa huduma za lugha.

IX. MAWASILIANO YA LUGHA RAHISI

Ni sera ambayo timu ya mawasiliano ya DPS inapitia nyaraka zote zinazosambazwa mara kwa mara ambazo zinatayarishwa na idara kwa ajili ya uwiano, usahihi na kuhakikisha kuwa maelezo ya maneno maarufu na yanayotumia kila siku iwezekanavyo. Nyaraka hizi zinazosambazwa mara kwa mara zinapitiwa na mtaalamu wa mada na timu ya mawasiliano kabla ya kuchapishwa.

Wafanyakazi wanaowajibika kwa utayarishaji wa nyaraka hizi wamepata mafunzo ya lugha rahisi. Nyaraka zinapitiwa kwa ajili ya ubayana kabla ya tafsiri na uhariri kufanywa inapohitajika. Nyenzo zote za uhamasishaji wa DPS zinapaswa kutumia kanuni za lugha rahisi:

- Maudhui yanaandikwa katika sentensi fupifupi.
- Maudhui yanapangiliwa kwa kutumia orodha, majedwali na vichwa.
- Maudhui yanaandikwa katika kauli tendi.
- Maudhui hayana istilahi.

X. MBINU MBADALA ZA MAWASILIANO

Mipango ya DPS inahimizwa kutathmini mahitaji ya umma kwa ajili ya mbinu na miundo mbadala ya mawasiliano na kubadilisha mahitaji hayo inapowezekana. Watu wasio na LEP wanaweza pia kunufaika kutokana na mbinu mbadala za mawasiliano. Watu kama hao ni pamoja na, lakini si tu, watu walio na matatizo ya kusikia, kuona, kuhisi, ukuaji na/au utambuzi na watu wasiojua kusoma na kuandika au walio na uwezo mdogo wa kusoma na kuandika.

JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA MPANGO WA UFUKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA

Mbinu mbadala za mawasiliano ni pamoja na, lakini si tu, rekodi za sauti na/au video, Breli, maandishi makubwa, na vielezo vya michoro ya maudhui ya maandishi.

XI. UFAAFU WA MILA NA ISIMU

Ili mawasiliano yafae, lazima yafae kimila a kiisimu. Mipango ya DPS inahimizwa kuendelea kutathmini na kuboresha ufaafu wa mila na isimu wa nyenzo na maelezo yao. Mipango ya DPS inahimizwa kujifunza kuhusu kanuni, mbinu na vidokezo vya kupata maoni kuhusu ufaafu wa mila na isimu ya mipango, huduma na maelezo.

XII. MAFUNZO YA WAFANYAKAZI

Mafunzo ya wafanyakazi kuhusu ufukiaji wa huduma za lugha yatajumuisha yafuatayo (1) majukumu ya kisheria ya DPS ili kutoa ufukiaji wa huduma za lugha; (2) rasilimali za DPS za kutoa huduma za ufukiaji wa lugha; (3) jinsi ya kufikia na kufanya kazi na wakalimani; (4) ufaafu wa mila na isimu; (5) jinsi ya kupata huduma za tafsiri; na (5) kudumisha rekodi za ufukiaji wa huduma za lugha zinazopewa watu wa LEP.

DPS itatoa mafunzo kwa waajiriwa wote walio kwenye Mpango huu wa Ufukiaji wa Huduma za Lugha na taratibu zinazohusika. DPS itatoa mafunzo ya kunoa ubongo baada ya kila mabadiliko ya Mpango wa Ufukiaji wa Huduma za Lugha. Rasilimali Watu atadumisha rekodi za mafunzo yote ya LEP yanayotolewa na atahifadhi nakala katika kila faili ya mafunzo ya mwajiriwa kwa mujibu wa ratibi za kuhifadhi rekodi zilizowekwa.

Wanafanyakazi wanaojibu simu za umma kwenye maeneo ya kupeleka ya VSP watapewa mafunzo ya ziada kama sehemu ya mipango yao ya mafunzo maalum.

XIII. MAJUKUMU YA WAFANYAKAZI

Lazima wafanyakazi wa DPS wafanye kila jitihada kutoa huduma za usaidizi wa lugha wanapokutana, au wanaweza kutarajia kukutana na watu wa LEP. Vilevile, lazima wafanyakazi wa DPS wachukue hatua zinazofaa za kutoa huduma za usaidizi wa lugha wanapopata ombi na mtu wa LEP ambaye angependa kufikia huduma au maelezo ya DPS. Wafanyakazi wantarajiwa kuwasiliana na wasimamizi wao kwa ajili ya mwongozo wakati wameshindwa kutimiza ombi la usaidizi wa lugha.

Wafanyakazi wa DPS hawapaswi kamwe kumnyima mtu wa LEP huduma ambaye anaomba usaidizi, wala kuhitaji mtu wa LEP kuleta mkalimani kama sharti la kupata usaidizi.

Wafanyakazi wa DPS watatumia zana zote ambazo zinafaa zilizopo, kama vile kadi za utambujaji wa lugha, wakati wanajaribu kubaini lugha ya msingi ya mtu wa LEP.

Watu wa LEP wanaweza kuamua kukubali huduma za LEP zinazotolewa na DPS bila malipo au wanaweza kuamua kutoa zao binafsi.

Wafanyakazi wa VSP wanatii SERA YA HUDUMA ZA MKALIMANI YA VSP-DIR-425 wakati huduma za usaidizi wa lugha zinapewa watu wa LEP.

Wafanyakazi watajaza fomu ya Ufuatiliaji wa Usaidizi wa Lugha ([Kiambatisho C](#)) wakati usaidizi wa lugha unaombwa na/au unatolewa.

XIV. UHIFADHI WA REKODI

Ripoti au nyaraka zozote zinazohitajika chini ya mpango huu wa ufukiaji wa huduma za lugha zitahifadhiwa na mwajiriwa anayekamilisha ripoti au nyaraka kwa miaka mitatu. Mbali na hayo, waajiriwa watasambaza nakala za nyaraka na ripoti kwa Title VI Coordinator kwa DPS.LanguageAccess@vermont.gov atakayehifadhi ripoti na nyaraka kwa mujibu wa sera za uhifadhi za Jimbo na serikali kuu.

XV. KUFUATILIA NA TATHMINI

DPS itatathmini Mpango huu kila mwaka na kuubadilisha inavyohitajika ili kuhakikisha kwamba shughuli za sasa za ufukiaji wa huduma za lugha ni za kisasa na zinakidhi mahitaji ya isimu ya umma.

Tathmini hii itajumuisha mchakato wa kupata maoni kutoka kwa washirika wa jamii na wanajamii. Mikakati ya tathmini inaweza kujumuisha, lakini si tu:

- Kufuatilia matumizi ya huduma za usaidizi wa lugha
- Uridhikaji wa huduma za usaidizi wa lugha
- Kufuatilia malalamishi ya ufukiaji wa huduma za lugha
- Dhana ya washirika wa jamii ya ufukiaji muhimu na/au vizingiti
- Mapengo ambapo huduma za usaidizi wa lugha hazikidhi mahitaji ya watu wa LEP
- Nambari na aina ya malalamishi na mwitikio wa shirika
- Mabadiliko ya Jimbo la demografia ya Vermont yanayohusiana na lugha, uwezo wa kusoma na kuandika, LEP na mambo ya mila

Matokeo ya tathmini yatatumiwa kufanya uamuzi wa Mipango ya Ufukiaji wa Lugha inayofuata.

XVI. TAFSIRI YA NYARAKA MUHIMU

Nyaraka muhimu au zile zinazotumika mara kwa mara zitatafsiriwa katika lugha inaweza kutumika sana. Mratibu wa Title VI atapanga ili kuwezesha nyaraka hizi zilizotafsiriwa kupatikana inapohitajika.

XVII. UTAYARI WAKATI WA DHARURA

Wakati wa migogoro ya dharura, DPS itatumia rasilimali zote zilizochezwa katika Mpango wa Ufukiaji wa Huduma za Lugha (mfano, kandarasi za wachuuzi, waajiriwa wa lugha mbili, Google Translate) kuhakikisha kuwa ujumbe muhimu umesambazwa kwa watu wa LEP katika jimbo zima. Vituo vya mawasiliano ya migogoro vitajumuisha, lakini si tu, mitandao ya jamii, vyombo vya habari, programu za mkononi na mifumo ya kupaza sauti.

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

Ukurasa wavuti wa Utayari wa Jamii ya VEM <https://vem.vermont.gov/preparedness> unatoa viungo vya nyaraka zifuatazo za utayari wa jamii kwa lugha ambazo si Kiingereza.

Kichwa cha Waraka	Lugha
Karatasi ya Maelezo kuhusu Cha Kufanya Ikiwa Tufani Inakuja	Kivietnamu, Kiswahili, Kihispania, Kisomali, Kiserbia-Kikroeshia, Kirusi, Kinepali, Kifaransa, Kiingereza, Kichina, Kibama, Kiarabu
Karatasi ya Maelezo kuhusu cha kufanya wakati Umeme Unakatika	Kiarebia, Kibama, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kinepali, Kirusi, Servo-Croatian, Kisomali, Kihispania, Kiswahili, Kivietnamu
Ukweli kuhusu Dhoruba ya Majira ya Baridi - Karatasi ya Maelezo	Kiarabu, Kibama, Kichina, Kiingereza, Kifaransa, Kinepali, Kirusi, Servo-Croatian, Kisomali, Kihispania, Kiswahili, Kivietnamu
Maratasi ya Maelezo Kabla na Baada ya Mafuriko	Kivietnamu, Kiswahili, Kihispania, Kisomali, Kiserbia-Kikroeshia, Kirusi, Kinepali, Kifaransa, Kiingereza, Kichina, Kibama, Kiarabu

[Ready.gov](#) ni kampeni ya huduma ya umma ya taifa iliyoungwa ili kuelimisha na kuwezesha umma kujitayarisha kwa ajili ya, kukabiliana na kupunguza hali za dharura. Lengo ni kuendeleza utayari kupitia ushirikishaji umma. Tovuti ina wiji inayoruhusu maudhui kutafsiriwa katika lugha kadhaa. Tovuti pia ina nyaraka, kama vile violezo vya [Mpango wa Mawasiliano ya Dharura ya Familia](#), kwa lugha za Kiingereza, Kihispania, Kichina Rahisi, Kichina cha Jadi, Kivietnamu, Kikorea na Kitagalogi.

XVIII. UHAMASISHAJI NA UFAHAMU WA UMMA KUHUSU HUDUMA ZA UFIKIAJI WA LUGHA

Ishara inayoonyesha kwamba wakalimani wapo bila malipo kwa watu wa LEP itawekwa katika maeneo yanayofaa kwenye vituo vya DPS. Ishara pia itaufahamisha umma jinsi ya kuwasilisha malalamishi kuhusu ufikiaji wa huduma za lugha.

Ishara itachapishwa katika lugha zifuatazo: Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Lugha Nyingine za Kihindi, Kichina, Kivietnamu, Kiarabu, Kirundi, Kilingala, Kinepali, Kiserbia-Kikroeshia, Kisomali na Kiswahili.

Rejelea [Kiambatisho E](#) kwa orodha ya vituo vya umma vya DPS ambapo ishara itawekwa.

XIX. UTARATIBU WA MAONI NA MALALAMISHI YA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA

Maoni kuhusu ufikiaji wa huduma za lugha yanaruhusiwa na kupokelewa kupitia kwa Mratibu wa Title VI.

JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA

Watu walio na malalamishi kuhusu ufikiaji wa huduma za lugha wanaweza kuyaelekeza kwa Mratibu wa Title VI ambaye ana jukumu la kufuatilia na kusuluhisha malalamishi ya ufikiaji wa huduma za lugha.

Watu wanaweza kutumia fomu ya Malalamishi ya Ufikiaji wa Huduma za Lugha ([Kiambatisho B](#)) kuwasilisha malalamishi yao. Fomu ya Malalamishi ya Ufikiaji wa Huduma za Lugha itapatikana katika lugha zifuatazo: Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Lugha Nyingine za Kihindi, Kichina, Kivietnamu, Kiarabu, Kibama, Kirundi, Kilingala, Kinepali, Kiserbia-Kikroeshia, Kisomali na Kiswahili. Lugha nyingine zitatafsiriwa zinapohitajika.

Ishara inayoeleza jinsi ya kuwasilisha malalamishi ya ufikiaji wa huduma za lugha itawekwa katika vituo vyote vya umma na kujumuishwa kwenye tovuti za DPS katika lugha zifuatazo: Kiingereza, Kifaransa, Kihispania, Lugha Nyingine za Kihindi, Kichina, Kivietnamu, Kiarabu, Kibama, Kirundi, Kilingala, Kinepali, Kiserbia-Kikroeshia, Kisomali na Kiswahili.

XX. MRATIBU WA TITLE VI

A. Madhumuni

Mratibu wa Title VI ana jukumu la huduma za usaidizi wa lugha na anasimamia utendakazi na utekelezaji wa mpango wa ufikiaji wa huduma za lugha.

B. Jina na Maelezo ya Mawasiliano

Mratibu wa Title VI wa DPS ni Naibu Kamishna wa Idara ya Usalama wa Umma (au mteule), ambaye anaweza kufikiwa kwa maelezo ya mawasiliano yanayofuata:

- Kwa simu kwenye (802) 244-8727
- Kwa barua pepe kwenye DPS.LanguageAccess@vermont.gov
- Kwa first class mail kwenye 45 State Dr, Waterbury Village Historic District, VT 05676

C. Kuripoti Mahusiano

Mratibu wa Title VI anaripoti kwa Kamishna wa Idara ya Usalama wa Umma.

D. Wajibu na Majukumu

Mratibu wa Title VI anaweza kusimamia wafanyakazi na utendakazi wa wakalimani na watafsiri wa waajiriwa na wasio waajiriwa, ikiwemo

- Kutambua wakalimani na watafsiri waliohitimu ili kujumuishwa katika hifadhidata ya wakalimani;
- Kubainisha mikakati ya kuhakikisha udhibiti wa ubora wa wakalimani na watafsiri;
- Mafunzo na kuwatathmini watu wa lugha mbili ikiwemo wafanyakazi wanaotoa huduma za usaidizi wa lugha;
- Kuwapa wakalimani, watafsiri na waajiriwa wa lugha mbili majukumu ya usaidizi wa lugha;
- Kudumisha orodha inayosasishwa mara kwa mara ya waajiriwa wa lugha mbili, wakalimani na watafsiri wote wa kandarasi inayojumuisha upatikanaji wao, lugha inayozungumzwa isiyo ya Kiingereza na maelezo ya mawasiliano;

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

- Kuunda mkakati wa ununuzi kwa ajili ya watoa huduma za usaidizi wa lugha wa kandarasi;
- Kutafuta ufadhili na rasilimali nyingine ili kusaidia huduma za ukalimani na tafsiri; usaidizi wa teknolojia na miundo msingi na wafanyakazi;
- Kutoa mchango katika masuala ya uundaji wa bajeti na ununuzi yanayohusiana na utekelezaji wa sera ya ufikiaji wa huduma za lugha na taratibu; na
- Kuratibu ununuzi kwa ajili ya fidia ya mkalimani na mtafsiri kwa huduma zilizotolewa.

Mratibu wa Title VI pia:

- Atahakikisha kuwa ishara inayosema kuwa wakalimani wanapatikana bila malipo kwa watu wa LEP imewekwa katika maeneo yanayofaa na katika lugha zinazozungumzwa sana.
- Atapitia nyaraka zilizopo na mpya zilizoundwa ili kuamua nyaraka muhimu na zinazopaswa kutafsiriwa na lugha ambazo nyaraka zinapaswa kutafsiriwa.
- Atapokea na kujibu malalamishi na maoni kuhusu huduma za DPS LEP.
- Atahakikisha michakato inayofaa imewekwa ili kutoa suluhisho la haraka na la usawa la malalamishi na maulizo kuhusu ubaguzi katika ufikiaji wa huduma, mipango na shughuli za DPS.
- Atatathmini mara kwa mara data ya demografia na rasilimali nyingine, ikiwemo data ya matumizi ya huduma za lugha zenye kandarasi na mashirika ya jamii ili kuamua ikiwa kuna nyaraka au lugha za ziada zinazofaa tafsiri.
- Atapitia mara kwa mara jitihada za DPS za kutoa ufikiaji muhimu kwa watu wa LEP na kuunda ripoti, taratibu mpya au kupendekeza marekebisho kwenye sera hii inavyofaa.

E. Mratibu Mteule wa Ufikiaji wa Huduma za Lugha wa Karibu

Mratibu mteule wa Ufikiaji wa Huduma za Lugha wa karibu pamoja na usaidizi wa Mratibu wa Title VI, anatumika kama rasilimali kwenye kitengo chake husika ili kuhakikisha kwamba watu walio na Ufasaha Kidogo wa Kiingereza (LEP) wana ufikiaji muhimu wa mipango na huduma za kitengo chao husika bila malipo kwa mtu wa LEP.

Jina na maelezo ya mawasiliano ya mratibu mteule wa ufikiaji wa huduma za lugha wa karibu kwa kila kitengo ni kama yafuatayo:

Kitengo	Jina na Maelezo ya Mawasiliano
Polisi ya Jimbo la Vermont	Wakurugenzi Wenza, Usimamizi wa Haki na Usawa na Masuala ya Jamii
Udhibiti wa Hali ya Dharura wa Vermont	Mkuu wa Kitengo cha Mipango au Mkurugenzi wa VEM
Kitengo cha Usalama wa Moto cha Vermont	Msaidizi wa Mkuu wa Moto na Afisa wa Elimu ya Umma
Maabara ya Uchunguzi ya Vermont	Mkurugenzi wa VFL
Kituo cha Habari za Uhalifu cha Vermont	Mkurugenzi wa VCIC

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

Kitengo	Jina na Maelezo ya Mawasiliano
Huduma za Teknolojia za Redio ya Vermont	Mkurugenzi wa VRTS
Fedha na Utawala wa DPS	Meneja wa Uendeshaji na Udhibiti wa Ndani

KIAMBATISHO A: SERA YA HUDUMA ZA UKALIMANI YA VSP-DIR-425

1.0 Madhumuni

- 1.1 Madhumuni ya sera hii ni kutoa miongozo ya kupata huduma za ukalimani kwa waajiriwa wa idara wanaoshiriki katika shughuli za idara.

2.0 Sera

- 2.1 Ni sera ya Vermont State Police kutoa huduma bora na za usawa kwa umma wote kwa kuwezesha mawasiliano na watu wasiozungumza Kiingereza kwa kutumia huduma za ukalimani inapohitajika.
- 2.2 Washirika wanapaswa kuzingatia Title VI ya Sheria ya Haki za Raia ya 1964 na kutumia huduma za mkalimani mtaalamu ana kwa ana au kwa njia ya simu inapohitajika kuzungumza na mtu aliyenafasaha kidogo wa Kiingereza.
- 2.3 Kwa mujibu wa sheria ya serikali kuu na ya jimbo, mashirika ya utekelezaji sheria yanahitajika kutoa huduma za ukalimani zinazostahiki kwa mtu yeyote anayehitaji. Washirika hawatawasiliana na mamlaka ya serikali kuu kwa ajili ya huduma za ukalimani, isipokuwa hali ya dharura bayana ihitajike na huduma za ukalimani zenye leseni hazipatikani kupitia njia nyingine yoyote.
- 2.4 Isipokuwa kimoja cha vighairi vifuatavyo kitumike, mshirika hatauliza kuhusu hali ya uhamiaji wa mtu ambaye anahitaji ukalimani:
- A. Mshirika anafanya kazi na wabia wa Serikali kuu katika mpango wa Stone Garden au mipango kama hiyo ya Serikali Kuu.
 - B. Hali ya uhamiaji wa raia ni muhimu kwa uchunguzi unaoendelea wa kosa la uhalifu. Ni muhimu kusisitiza kwamba mshirika hapaswi kutumia sifa za mtu kuwa sababu za kuuliza kuhusu hali ya uhamiaji.

3.0 Utaratibu

- 3.1 Wakati mshirika wa Idara au mwajiriwa anahitaji kuwasiliana na mtu asiyezungumza Kiingereza na imetambuliwa kwamba mkalimani anahitajika na hakuna trupa anayezungumza lugha hiyo, huduma ya ukalimani iliyoidhinishwa na Idara itatumwa. Idhini ya mapema ya msimamizi si muhimu.
- 3.2 Huduma za ukalimani zinapatikana kwa njia ya simu na mkalimani ambaye anatumika kama daraja kati ya mzungumzaji asiye wa Kiingereza na mshirika wa Idara au mwajiriwa. Ufuatao ni mchakato wa kuwasiliana na mkalimani:
- A. Jaribu kutambua lugha ya mzungumzaji asiye wa Kiingereza.
 - B. Wasiliana na usimamizi kwa njia ya simu mahali ambapo msimamizi atamuunganisha trupa na huduma ya ukalimani. Nambari ya simu ya mawasiliano na nambari ya akaunti ziko kwenye faili kwa kila PSAP.

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

- C. Kisha msimamizi ataweka mtu huyo ili awasiliane kwa simu moja kwa moja na mkalimani. Mawasiliano kati ya Trupa, mtu asiyezungumza Kiingereza na mkalimani yatafanyika kwa njia ya simu.
- D. Kwa madhumuni ya ufuatiliaji na bili, Fomu ya Ufuatiliaji wa Huduma za Ukalimani itajazwa na msimamizi na kuwasilisha kwa Msimamizi wa PSAP kila wakati huduma za ukalimani zinapotumiwa. Fomu hii inapatikana katika kila PSAP na kwenye Power DMS.
- E. Kwa mahojiano ya ana kwa ana yaliyopangwa ambayo yameratibiwa mapema, Muungano wa Waafrika Wanaoishi Vermont (Association of Africans Living in Vermont, AALV) na Vermont Refugee Resettlement Program (VRRP) pia wana wakalimani. Maelezo ya mawasiliano ya mashirika haya yako kwenye faili katika kila PSAP. Ili kuwezesha kuratibu, mashirika haya yanapaswa kutumiwa ilani ya mapema iwezekanavyo.
 - 1. Mkalimani wa Vermont Refugee Resettlement Program atahitaji fomu ya mawasiliano iliyo kwenye faili katika Power DMS, itumiwe kurekodi utumiaji wa wakalimani wao. Hakuna ada kwa ajili ya huduma zao ambazo zitatozwa idara. Wakati mwingine, huenda wakawa na wakalimani baada ya saa kadhaa au kunapokuwa na haja.

3.3 Vikwazo

- A. Matumizi ya huduma za ukalimani zilizoidhinishwa na Idara yanaidhinishwa na shughuli rasmi za Idara pekee. Matumizi mengine yoyote yanapigwa marufuku kabisa na huenda yakasababisha hatua ya nidhamu kuchukuliwa kwa hadi na ikiwemo usimamishwaji kazi.

Kuanzia tarehe 30 Januari, 2019

Vermont State Police Manual inatoa mwongozo wa ndani tu wa Vermont State Police. Haijakusudiwa, haitategemewi na huenda isitegemewe kuunda haki yoyote halisi au ya utaratibu na ya kutekelezeka kisheria na mhusika yeyote katika kesi yoyote ya raia, uhalifu au utawala. Jaijakususidiwa na haitumiki kwa kesi yoyote ya uhalifu wala raia nje ya kesi za ndani ya Idara. Hakuna sera iliyojumuishwa katika chapisho hili ianapswa kufasiriwa kuwa kuunda kiwango cha juu cha sheria ya usalama au utunzaji katika hali ya ushahidi kuhusiana na madai ya mhusika mwingine.

KIAMBATISHO B: FOMU YA MALALAMISHI YA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA

Kamilisha na urejeshe kwa:

Mratibu wa Title VI, Idara ya Usalama wa Umma

Bwa Barua pepe: DPS.LanguageAccess@vermont.gov

**Kwa First Class Mail: 45 STATE DR
WATERBURY VILLAGE HISTORIC DISTRICT,
VT 05676**

JINA LAKO LA KWANZA	JINA LAKO LA MWISHO
ANWANI YAKO YA BARUA	
NAMBARI YAKO YA SIMU	ANWANI YAKO YA BARUA PEPE
JE, UNAPENDELEA KUWASILIANA KWA LUGHA GANI?	
JE, UNAHITAJI UKALIMANI WA LUGHA?	IKIWA NDIYO, LUGHA GANI?

Ikiwa unalalamika kuhusu mtu, tafadhali bainisha:

JINA LA MTU	CHEO CHA MTU	KITENGO CHA MTU

ELEZA SABABU YA KULALAMIKA (TUMIA KARATASI YA ZIADA IKIHITAJIKA)

ELEZA JINSI UNAVYOTAKA MALALAMISHI YAKO YASULUHISHWE (TUMIA KARATASI YA ZIADA IKIHITAJIKA)

Maelezo yaliyo hapo juu ni ya kweli na kamilifu kadri ya ufahamu na imani yangu.

SAHIHI YAKO	TAREHE
--------------------	---------------

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

**KIAMBATISHO C: FOMU YA IDARA YA UFUATILIAJI WA USAIDIZI WA LUGHA YA
USALAMA WA UMMA**

MAAGIZO: Fomu hii ilitumiwa kufuatilia maombi ya na utoaji wa huduma za usaidizi wa lugha. Tafadhali jaza fomu kwa kila ombi na/au utoaji wa huduma za usaidizi wa lugha

Tuma fomu iliyojazwa kwa DPS.LanguageAccess@vermont.gov na uhifadhi nakala kwa ajili ya rekodi zako kwa miaka mitatu.

JINA LA MWAJIRIWA	KITENGO	ANWANI YA BARUA PEPE

LUGHA ILIYOOMBWA	TAREHE YA OMBI
MPANGO AU HUDUMA AMBAYO USAIDIZI WA LUGHA ULIOMBWA	

NJIA YA MAWASILIANO

Simu Kuingia bila miadi Miadi Nyingine (tafadhali bainisha)

Huduma ya Usaidizi wa Lugha	Imeombwa	Imetolewa
Ukalimani	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
Tafsiri	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
Mwajiriwa wa lugha mbili	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
Lugha ya Ishara	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
Tafsiri ya kiotomatiki	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

Huduma ya Usaidizi wa Lugha	Imeombwa	Imetolewa
Mbinu Mbadala za Mawasiliano (Tafadhali bainisha)	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>
Nyingine (Tafadhali bainisha)	<input type="checkbox"/>	<input type="checkbox"/>

Ikiwa huduma za usaidizi wa lugha ziliombwa na hazikutolewa, tafadhali elezea sababu

SAHIHI YA MWAJIRIWA	TAREHE
----------------------------	---------------

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

KIAMBATISHO D: FOMU YA OMBI LA MKALIMANI YA AALVI



**Interpreter Request / Appointment Form
AALVInterpret**

Order #:

Department _____
 Division/ Program _____
 Program Code _____
 Address: _____
 Contact Name _____
 Phone # _____
 e-Mail _____

Appointment Date _____
 Start Time _____
 Location _____
 Language _____

Was a reminder call Requested by the provider?
 Yes No

Date of contact	Time of contact	Name of person contacted

If no contact was made please complete the following:

Not a working number	Left a voice message	Date of message

Arrival Time of Interpreter	INTERPRETER CHECK-IN To be completed by PROVIDER ONLY

Client First Name	Client Last Name	Start Time	End Time	# of Hours	Approved By (signature)
					(Print Name Here)

AALVInterpret
 20 Allen St.
 Burlington, VT 05401
 Tel: 802-985-3106
 Fax: 802-881-0521

Notes:

Interpreter Name: _____

Interpreter Signature: _____

Ilirekebishwa tarehe 17 Aprili, 2020

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

KIAMBATISHO E: VITUO VYA UMMA VYA DPS

Kitengo	Kituo	Nchi	Lugha Kuu¹
Usalama wa Moto	Waterbury Central Office Division of Fire Safety 45 State Drive Waterbury, VT 05671	Washington	Kifaransa, Kiserbia- Kikroeshia, Kijerumani, Kivietnamu, Kihispania, Lugha Nyingine (14%)
	Division of Fire Safety 56 Howe Street, Building A, Suite 200 Rutland, VT 05701-3449	Rutland	Kichina, Kifaransa, Kitagalogi, Kihispania, Kijapani, Lugha Nyingine (40%)
	Barre Regional Office 1311 U.S. Route 302 - Suite 500 Berlin, VT	Washington	Kifaransa, Kiserbia- Kikroeshia, Kijerumani, Kivietnamu, Kihispania, Lugha Nyingine (14%)
	Division of Fire Safety 100 Mineral Street, Suite 307 Springfield, VT 05156-3168	Windsor	Kihispania, Kifaransa, Kikorea, Kichina, Kijerumani, Lugha Nyingine (17%)
	Division Fire Safety 380 Hurricane Lane, Suite 101 Williston, VT 05495	Chittenden	Kihindi Kingine, Kivietnamu, Kifaransa, Kichina, Kihispania, Lugh Nyingine (43%)
	Vermont Fire Academy 93 Davison Drive Pittsford, VT 05763	Rutland	Kichina, Kifaransa, Kitagalogi, Kihispania, Kijapani, Lugha Nyingine (40%)

¹ Chanzo: U.S. Census 2011-2015 American Community Survey Data Table B16001

**JIMBO LA VERMONT – IDARA YA USALAMA WA UMMA
MPANGO WA UFIKIAJI WA HUDUMA ZA LUGHA**

Kitengo	Kituo	Nchi	Lugha Kuu¹
Polisi ya Jimbo la Vermont	Williston Barracks - Troop A 2777 St George Rd Williston, VT, 05495	Chittenden	Kihindi Kingine, Kivietnamu, Kifaransa, Kichina, Kihispania, Lugha Nyingine (43%)
	St Albans Barracks - Troop A 140 Fisher Pond Road St Albans, VT, 05478	Franklin	Kifaransa, Kihispania, Kipolandi, Kitagalogi, Kijerumani, Lugha Nyingine (5%)
	Middlesex Barracks - Troop A 1080 US Route 2 Middlesex, VT, 05602	Washington	Kifaransa, Kiserbia- Kikroeshia, Kijerumani, Kivietnamu, Kihispania, Lugha Nyingine (14%)
	St Johnsbury Barracks - Troop A 1068 US Route 5, Suite #1 St Johnsbury, VT, 05819	Caledonia	
	Derby Barracks - Troop A 35 Crawford Road PO Box 410 Derby, VT, 05829	Orleans	
	Westminster Barracks - Troop B 1330 Westminster Heights Rd Putney, VT, 05346	Windham	
	Royalton Barracks - Troop B 2011 VT Route 107 Bethel, VT, 05032	Windsor	Kihispania, Kifaransa, Kikorea, Kichina, Kijerumani, Lugha Nyingine (17%)
	Shaftsbury Barracks - Troop B 96 Airport Road Shaftsbury, VT, 05262	Bennington	
	Rutland Barracks - Troop B 124 State Place Rutland, VT, 05701-9332	Rutland	Kichina, Kifaransa, Kitagalogi, Kihispania, Kijapani, Lugha Nyingine (40%)
	New Haven Barracks - Troop B S.L. P 83 New Haven, VT, 05472	Addison	